# Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles
# Idhini ya Huduma (Kiwango cha 3)

**Tafadhali jaza taarifa hapa chini, tia saini na uirudishe kwenye shule ya mtoto wako.**

**Jina la Kwanza na la Mwisho la Mtoto:** ________________________________ **Tarehe ya Kuzaliwa**: __________

## Ni matibabu gani yanayotolewa kupitia Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles wa mtoto wangu?

Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles wa shule yako unatoa uchunguzi wa meno, usafishaji wa meno, vanishi ya floraidi na silver diamine fluoride (SDF) (kwa Kiingereza). **Ili kupokea matibabu ya SDF, unahitaji kujaza fomu ya idhini ya ziada; soma zaidi kuhusu matibabu ya SDF kwenye fomu hiyo.**

Tunapendekeza mtoto wako apokee huduma kupitia hospitali ya meno mnakopata huduma, ikiwa unayo, badala ya kupitia Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles wa shule yako.

## Idhini ya Matibabu:

☐ **Ndiyo, ningependa mtoto wangu ashiriki katika Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles.** Ninaelewa kwamba ikiwa kuna daktari wa meno aliyeorodheshwa kwenye fomu hii, atapata ripoti ya matokeo kutoka kwa mtaalamu wa usafi wa meno wa 802 Smiles. Ninaelewa kuwa mtoto wangu anaweza kupokea huduma yoyote au zote zifuatazo kulingana na tathmini ya mtaalamu wa usafi wa meno wa 802 Smiles, bila kushauriana na daktari wa meno:

- uchunguzi wa meno
- usafishaji wa meno
- vanishi ya floraidi
- silver diamine fluoride

☐ **Hapana, singependa mtoto wangu ashiriki katika Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles.**

## Idhini ya Kushirikiwa kwa Taarifa:

Kushiriki na daktari wa meno wa mtoto wako: Ikiwa mtoto wako ana daktari wa meno kwenye kumbukumbu zetu na uchague kupata huduma za meno kupitia Mpango wa 802 Smiles, taarifa kuhusu huduma zilizotolewa zitashirikiwa naye. **Kushiriki taarifa hizi ni lazima:**

☐ Ndiyo**, ningependa taarifa za mtoto wangu zishirikiwe na daktari wake wa meno aliye kwenye kumbukumbu.**

☐ **Hapana, singependa taarifa za mtoto wangu zishirikiwe na daktari wake wa meno aliye kwenye kumbukumbu. Ninaelewa mtoto wangu hatapokea huduma za meno kupitia Mpango wa 802 Smiles.**

Kushirikiwa na Idara ya Afya ya Vermont: Idara ya Afya ya Vermont ingependa kutumia taarifa za mtoto wako kutathmini ufanisi wa mpango huu. Je, pia unatoa ruhusa kwa mtaalamu wa usafi wa meno wa 802 Smiles kushiriki rekodi za matibabu ya meno za mtoto wako na Idara ya Afya ya Vermont? **Kushiriki huku ni hiari:**

☐ **Ndiyo, ninaruhusu** mtaalamu wa usafi wa meno wa 802 Smiles kushiriki **rekodi za meno za mtoto wangu** na Idara ya Afya ya Vermont.

☐ **Hapana, siruhusu** mtaalamu wa usafi wa meno wa 802 Smiles **kushiriki rekodi za meno za mtoto wangu** na Idara ya Afya ya Vermont.

Tafadhali teua hapa ikiwa wewe ni **mzazi mlezi**, au ikiwa mnashirikiana **na mtu mwingine katika ulezi wa mtoto huyu**: ☐

Saini ya Mzazi/Mlezi: ______________________________________ Tarehe: __________

Jina Lililoandikwa la Mzazi/Mlezi: ________________________________________________

**Ikiwa unampa mtoto wako ruhusa ya kushiriki katika Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles, tafadhali endelea kwenye ukurasa unaofuata.**

# Mpango wa Afya ya Meno wa 802 Smiles
# Idhini ya Huduma (Kiwango cha 3)

## Historia ya meno ya mtoto:

Je, ni lini mtoto wako alipata huduma za meno hivi karibuni zaidi?

○ Ndani ya mwaka mmoja uliopita ○ Zaidi ya mwaka mmoja uliopita ○ Hajawahi kuhudumiwa na daktari wa meno

Je, daktari wa meno wa mtoto wako ni nani ikiwa anaye? ________________________________________

Mtoto wako anatumia aina gani ya bima ya meno? Hakuna mtoto atakayenyimwa huduma kwa sababu hana bima. Kumbuka kwamba mtaalamu wa usafi wa meno wa 802 Smiles anaweza kutoza bima ya Medicaid kwa huduma zinazotolewa kwa mtoto wako.

○ Medicaid/Dr. Dynasaur - Nambari ya kitambulisho cha Medicaid cha mtoto wako: ___________________
○ Bima ya meno ya kibinafsi (yaani, Delta Dental) ○ Tricare
○ Hana Bima ○ Nyingine ___________________
○ Sijui

Je, mtoto wako ana mizio yoyote? (yaani, mzio wa dawa, chakula, ulimbo wa mpira, madini ya fedha, nk.) ○ Ndiyo ○ Hapana

Ikiwa ndiyo, ni ya aina gani? _________________________________________________________________

## Historia ya matibabu ya mtoto:

Je, mtoto wako ana ugonjwa au ulemavu wa kimwili, kiakili, kujifunza au wa kihisia?

○ Ndiyo ○ Hapana ○ Sijui ○ Singependa kusema

Ikiwa ulijibu ndiyo katika swali la awali, tunawezaje kumtunza mtoto wako wakati wa ziara yake ya meno?__________________________________________________________________________________________

## Maelezo ya hiari ya demografia:

**Jinsia aliyopewa alipozaliwa:** ○ Wa Kiume ○ Wa Kike ○ Asiye na Jinsia Maalum ○ Singependa kujibu

Swali linalofuata linauliza kuhusu utambulisho wa rangi ya ngozi na kabila la mtoto wako. Tunauliza swali hili kwa sababu tunataka kuhakikisha mpango wetu unahudumia watu wa rangi zote za ngozi na makabila yote. Tunaelewa kwamba huenda machaguo ya jibu yasiwakilishe kwa usahihi utambulisho wa mtoto wako.

**Ni lipi kati ya yafuatayo linalofafanua mtoto wako vyema zaidi? (tafadhali teua yote yanayohusika)**

○ Muabenaki au utambulisho mwingine wa Mzaliwa wa Marekani au Alaska

○ Muasia au Muasia Mmarekani, kwa mfano, Mchina, Muasia Mhindi, Mnepali au Mvietinamu

○ Mweusi au Mmarekani wa Kiafrika

○ Mhispania au Mlatino, Mlatina au Mlatinx, kwa mfano, Mmeksiko, Mvenezuela au Mbrazili

- ○ Mashariki ya Kati au Afrika ya Kaskazini (orodha imeendelezwa kwenye ukurasa unaofuata)
- ○ Mzaliwa wa Hawaii au Kisiwa kingine cha Pasifiki
- ○ Mzungu au Mlaya Mmarekani
- ○ Rangi au kabila la ziada, tafadhali taja: ____________________________
- ○ Singependa kujibu

Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa tujue kuhusu mtoto wako?

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

**Rudisha fomu iliyojazwa na iliyosainiwa kwa shule ya mtoto wako.**